**Ndugu zangu Waislamu wa Afrika ya mashariki,**

**Hotuba yetu ya leo ni kwa anwani:**

# إنسانيةُ الحضارةِ الإسلامية

# "Utu wa ustaarabu wa Kiislamu"

**kutoka Wizara ya Waqfu ya Misri**

**Imefasiriwa na**

**Profesa.Ayman Alasar**

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote, anayesema katika Qur'ani Tukufu:

"يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ"

**"Enyi watu mcheni Mwenyezi Mungu Mola wenu ambaye amewaumba nyinyi kutokana na nafsi moja",** na ninashuhudia kwamba hakuna Mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kwamba Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni mja na Mtume wake, Ewe Mwenyezi Mungu msalie, mpe salamu na umbariki yeye, Familia yake, Masahaba zake, na Kila atakayewafuata kwa wema mpaka Siku ya Malipo.

**Amma bado,,,**

Uislamu umesimamisha ustaarabu uliofikia kiwango kikubwa cha maadili mema ya kibinadamu na ukamilifu wake, pia umeweka kwa wanadamu njia ya upendo, udugu, uadilifu na usawa kupitia mfumo wa kimaadili na kistaarabu unayowakusanya watu bila ya kuwatengenesha,

na unayojenga bila ya kubomoa, ili kafanikisha usalama, amani na kheiri kwa watu wote.

Ustaarabu wa Kiislamu umechukua misingi yake ya kiutu kutokana na Quran Tukufu pamoja na Sunna za Mtume S.A.W ambapo misingi hiyo miwili ndio vyombo vilivyobeba misingi mikubwa ya kiutu, ambapo Mola wetu Mtukufu Anasema:

**{يَاأَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَى وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ}**

{**Enyi watu, hakika sisi tumekuumbeni nyinyi kutokana mwanamme na mwanamke, na tukawafanyeni kuwa mataifa na makabila mbalimbali ili mpate kufahamiana, kwa hakika mbora wenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule mche-Mungu zaidi kwenu, hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye habari**}. Mwanadamu ni mwenye kukirimiwa kwa ukarimu wa Mwenyezi Mungu kwake bila ya kuangalia kabila, rangi, au dini yake, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

**{وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ}**

{**Kwa hakika tumemkirimu mwanadamu**} na Mtume wetu S.A.W anasema:

**(كُلُّكُمْ لِآدَمَ، وَآدَمُ مِنْ تُرَابٍ)**

**“Nyinyi nyote munatokana na Adamu na Adamu ametokana na udongo”** pindi siku moja lilipopitishwa jeneza mbele ya Mtume wetu S.A.W akasimama, basi akaambiwa kwamba jeneza lile ni la Myahudi, wakati hii Mtume S.A.W akasema: **“Je, si mwanadamu?”.**

Miongoni mwa sura za ubinadamu wa ustaarabu wa Kiislamu ni kukubali kwake kwa uwazi msingi wa uhuru wa kuamini usiokubali maelezo zaidi, pia uhuru wa kuendesha na kusimamisha ibada za kidini na kuzilinda nyumba za ibada kwa watu wote, pia kupinga kwake aina zote za kulazimishana kwa nguvu na ugaidi katika dini, ambapo Mola wetu Mtukufu Anasema:

{لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ}

{**Hakuna kulazimishana kwa nguvu ndani ya dini**} na Anasema tena Mola Mtukufu:

{وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَآمَنَ مَن فِي الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا أَفَأَنتَ تُكْرِهُ النَّاسَ حَتَّى يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ}

{**Lau Angetaka Mola wako basi wangeamini watu wote duniani, hivi wewe unawalazimisha watu kwa nguvu ili wawe Waumin**} pia Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema tena:

{فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنتَ مُذَكِّرٌ * لَّسْتَ عَلَيْهِم بِمُصَيْطِرٍ}

{**Kumbusha kwani wewe ni mkumbushaji * hakuwa wewe kwao mwenye kuwatenza nguvu kwenye dini**}, pia Mola wetu Mtukufu anasema:

{إِنْ عَلَيْكَ إِلا الْبَلاغُ}

{**Ni juu yako kufikisha**}.

Pia miongoni mwa pande zake muhimu za kibinadamu ni: Huruma kwa wanyonge, kuwaheshimu wazee, na kuwapa haki zao zote kwa ukamilifu bila ya upungufu, ambapo Mtume wetu S.A.W anasema:

(إِنَّمَا يَنْصُرُ اللَّهُ هَذِهِ الأُمَّةَ بِضَعِيفِهَا، بِدَعْوَتِهِمْ، وَصَلاتِهِمْ، وَإِخْلاصِهِم)

**“Hakika Mwenyezi Mungu anaunusuru Umma huu kutoka na wale wanyonge wake kwa maombi yao swala zao na utakasifu wao wa maombi yao”,** pia Mtume wetu S.A.W anasema:

**(لَيْسَ مِنَّا مَنْ لَمْ يَرْحَمْ صَغِيرَنا، ويُوَقِّرْ كَبِيرَنا)**

**“Si miongoni mwetu yule asiye na huruma kwa wadogo wetu na kuwaheshimu wakubwa wetu”,** na siku moja Swahaba Omar Ibn Khattab alipopita kwa mtu mmoja mzee miongoni mwa watu wa kitabu akiwa anaomba misaada kutoka watu, basi Omar R.A akasema: Hatukukufanyia uadilifu katika ujana wako, kisha tukakupoteza katika uzee wako, kisha akampa kutoka hazina ya Waislamu kile kinachohitaji. pia Mtume S.A.W anasema:

**(الرَّاحِمُونَ يَرْحَمُهُمُ الرَّحْمَنُ ارْحَمُوا مَنْ فِي الْأَرْضِ يَرْحَمْكُمْ مَنْ فِي السَّمَاءِ)**

**“Watu wenye huruma huruhumiwa na Mwenyezi Mungu, basi mwaruhumuieni waliomo ardhini mutaruhumiwa kutokana na aliyepo mbinguni”.**

Ninaisema kauli yangu hii na ninamwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu msamaha kwa ajili yangu na yenu.

*********

Ndugu zangu waislamu tunazungumza katika hotuba yetu ya pili juu ya **"kupanuka utu wa ustaarabu wa Kiislamu"**

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote, na ninashuhudia kwamba hakuna Mungu anaystahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kwamba Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni mja na Mtume wake, Ewe Mwenyezi Mungu msalie, mpe

salamu na umbariki yeye, Familia yake, Masahaba zake, na Kila atakayewafuata kwa wema mpaka Siku ya Malipo.

**Ndugu zangu Waislamu:**

Hakika utu na ubinadamu wa ustaarabu wa Kiislamu haukusimama kwenye mipaka ya kutendeana na watu tu, bali umepanuka hadi kufikia kutendeana mwanadamu kwa wanyama, dalili kubwa ya hilo ni pale Mtume wetu Muhammad S.A.W alipoathirishwa wakati alipoingia bustani ya mitende ya kwa mtu miongoni mwa watu wa Madina alipomwona ngamia anayeonesha upole kwa Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) huku macho yake yakiwa yanateremsha machozi kutokana na alichofanyiwa na mlezi wake. Mtume akamfuta machozi yake, basi ngamia akanyamaza, kisha Mtume akauliza: **"Ni ngamia wa nani huyu? Wakati hii akaja kijana kutoka watu wa Madina akasema ni wangu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mtume akasema, kwanini hamchi Mwenyezi Mungu katika mnyama huyu ambaye Mwenyezi Mungu amekupa, kwani amenishtakia kuwa wewe unamtesa kwa njaa".**

Kama tulivyoona Mtume wetu S.A.W ghadhabu wa ndege alipokasirika kwa sababu ya ndegu mdogo aliyekuwa na watoto wake wawili kisha mmoja akachukuliwa, wakati hii Mtume S.A.W akauliza: **"Ni nani aliyemchukulia mtoto wa ndege huyu? Mrudisheni mtoto wake kwake".**

Wanadamu wote wanahitaji sana kufanikisha misingi hii ya utu na ubinadamu, ambayo ustaarabu wetu wa Kiislamu imesifiwa nayo kupitia kipindi chote cha historia.

**Ewe Mwenyezi Mungu ujaalie nchi yetu ya Misri yenye ustawi na nchi zengine za ulimwengu wa Kiarabu na Kiislamu.**

**والسلام عليكم ورحمة الله وبركاته**